Tarehe 04.06.2021

MAZINGIRA

MWANANCHI UK 19

# Uharibifu wa mazingira wapunguza samaki Mtera

Lwitiko Mwamakula, Mwananchi

Mpwapwa. Baraza la Madiwani wilayani Mpwapwa limeelezwa uharibifu wa mazingira kwenye Bwawa la Mtera umesababisha upungufu wa samaki na kushuka mapato ya halmashauri.

Hayo yalielezwa na diwani wa Mtera, Robert Maulya kwamba kutokana na uharibifu wa mazingira, samaki wamepungua na hivyo kushusha mapato ya halmashauri yanayotokana na uvuvi wa samaki.

Alisema kutokana na hali hiyo, kuna haja ya kuunganisha nguvu kati ya wanasiasa, jamii na viongozi wa Serikali kupambana na uharibifu wa mazingira ili kunusuru bwawa hilo.

Diwani huyo alisema wanasiasa pia wanatajwa katika uharibifu wa mazingira wa moja kwa moja au wa kuwakingia vifua wale wanaohusika katika uharibifu huo.

Mwenyekiti wa halmashauri hiyo, George Fuime alisema kwa sasa Mpwapwa ni miongoni mwa wilaya ambazo zimeanza kuathirika moja kwa moja na matokeo ya uharibifu wa mazingira, ikiwamo kutanuka kwa korongo la Shaban Robert linalosababisha baadhi ya nyumba za watu kusombwa na miundombinu ya madaraja na barabara kuharibika kwa kiasi kikubwa.

**"Kwa hali ilivyo ni lazima jamii na viongozi kuanzia ngazi za chini kupambana na uharibifu wa mazingira."**

Mkuu wa Wilaya ya Mpwapwa, Jabir Shekimweri



Hivyo alisema ni lazima kama wilaya kuongeza nguvu katika utunzaji na uhifadhi wa mazingira kwa kushughulikia vyanzo vikuu vya tatizo hilo. Kwa upande wake, Mkuu wa Wilaya ya Mpwapwa, Jabir Shekimweri alisema kwa hali ilipofikia ni lazima jamii na viongozi wote kuzungumza lugha moja katika utunzaji wa mazingira katika wilaya yake.

Alisema historia inaeleza Wilaya ya Mpwapwa ilikuwa inaongoza kwa kuwa na mazingira rafiki na mazuri kutokana na misitu mikubwa, hali ya hewa nzuri ambayo iliwafanya wakoloni kujenga ngome yao humo.

Pia alisema usimamizi mbovu wa sheria unashawishi waharibifu hao kutokuwa na woga wa kutenda makosa, siasa mbovu, rushwa kwa baadhi ya watendaji na kuyafumbia macho matendo hayo.

Alisema mikakati ya wilaya ni kuunda kamati za udhibiti wa uharibifu wa mazingira kuanzia ngazi ya serikali za vijiji na kuanzisha mahakama inayotembea ili kuongeza kasi ya utoaji adhabu kwa wahusika.

Scanned with CamScanner

# Wafugaji watakiwa kufuata kanuni za ufugaji- Serikali

NA IMMACULATE RUZIKA,DODOMA

SERIKALI kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi imewashauri wafugaji wafuge kwa kuzingatia Kanuni za ufugaji ili kukabiliana na mabadiliko ya Tabia Nchi.

Aidha Wizara hiyo imewataka wafugaji kuacha kufuga kiholela kwani Mifugo ikiachwa hovyo usababisha mmomonyoko wa udongo na uchafuzi wa mazingira.

Akizungumza katika maonesho ya wiki ya mazingira yanayoendelea Jijini hapa Kaimu Mkurugenzi Msaidizi Ugani Mifugo wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi Dkt. Kejeri Gillaa alisema wamekuwa wakitoa Elimu kwa wafugaji yankutunza mazingira.

" Sisi kama Wizara husika,tumekuwa tukitoa elimu kwa wafugaji wafuge kwa kuzingatia utunzaji na uhifadhi wa mazingira, kwani inawezekana" alisema Gillaa.

Alisema kuwa wafugaji wanaweza kuchafua mazingira kwa kumwaga kinyesi cha Mifugo ovyo pamoja na watu wa machinjio wamkuwa wakitupa ovyo uchafu unatokana na Mifugo iliyochinjwa.

Aidha Gillaa alisema wamekuwa wakitoa ushauri kwa wafugaji wafuge kwa kutima Mifugo chotara kwani ndio Wana himili mabadiliko ya Tabia Nchi yanayotokea.

"Mifugo ya chotara ni mchanganyiko wa mbegu ya kisasa na kienyeji, hivyo mchanganyiko huo unahimili mabadiliko ya Tabia Nchi hali inayopelekea Mifugo kuwa na Afya na kutoa maziwa mengi", alisema Kaimu Mkurugenzi huyo.

Kaimu Mkurugenzi huyo alisema katika kuhakikisha wafugaji wanapata malisho mazuri,Wizara ina mashamba ya kuzalisha mbegu Bora za malisho ambazo wamekuwa wakisambaza katika maeneo mbalimba hapa nchini.

Tanzanite Uk. 2
Tarehe 04/06/2021

Scanned with CamScanner

# Wafugaji watakiwa kufuata Kanuni za ufugaji- Serikali

**NA IMMACULATE RUZIKA-DODOMA**

SERIKALI kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi imewashauri wafugaji wafuge kwa kuzingatia Kanuni za ufugaji ili kukabiliana na mabadiliko ya Tabia Nchi.

Aidha Wizara hiyo imewataka wafugaji kuacha kufuga kiholela kwani Mifugo ikiachwa hovyo usababisha mmomonyoko wa udongo na uchafuzi wa mazingira.

Akizungumza katika maonesho ya Wiki ya mazingira yanayoendelea Jijini hapa Kaimu Mkurugenzi Msaidizi Ugani Mifugo wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi Dkt. Kejeri Gillaa alisema wamekuwa wakitoa Elimu kwa wafugaji yankutunza mazingira.

" Sisi kama Wizara husika,tumekuwa tukitoa elimu kwa wafugaji wafuge kwa kuzingatia utunzaji na uhifadhi wa mazingira, kwani inawezekana" alisema Gillaa.

Alisema kuwa wafugaji wanaweza kuchafua mazingira kwa kumwaga kinyesi cha Mifugo ovyo pamoja na watu wa machinjio wamkuwa wakitupa ovyo uchafu unatokana na Mifugo iliyochinjwa.

Aidha Gillaa alisema wamekuwa wakitoa ushauri kwa wafugaji wafuge kwa kutima Mifugo chotara kwani ndio Wana himili mabadiliko ya Tabia Nchi yanayotokea.

" Mifugo ya chotara ni mchanganyiko wa mbegu ya kisasa na kienyeji, hivyo mchanganyiko huo unahimili mabadiliko ya Tabia Nchi hali inayopelekea Mifugo kuwa na Afya na kutoa maziwa mengi", alisema Kaimu Mkurugenzi huyo.

Kaimu Mkurugenzi huyo alisema katika kuhakikisha wafugaji wanapata malisho mazuri,Wizara ina mashamba ya kuzalisha mbegu Bora za malisho ambazo wamekuwa wakisambaza katika maeneo mbalimbali hapa nchini.

Scanned with CamScanner

# Wafugaji watakiwa kufuata kanuni za ufugaji- Serikali

**NA IMMACULATE RUZIKA,DODOMA**

SERIKALI kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi imewashauri wafugaji wafuge kwa kuzingatia Kanuni za ufugaji ili kukabiliana na mabadiliko ya Tabia Nchi.

Aidha Wizara hiyo imewataka wafugaji kuacha kufuga kiholela kwani Mifugo ikiachwa hovyo usababisha mmomonyoko wa udongo na uchafuzi wa mazingira.

Akizungumza katika maonesho ya wiki ya mazingira yanayoendelea Jijini hapa Kaimu Mkurugenzi Msaidizi Ugani Mifugo wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi Dkt. Kejeri Gillaa alisema wamekuwa wakitoa Elimu kwa wafugaji yankutunza mazingira.

" Sisi kama Wizara husika,tumekuwa tukitoa elimu kwa wafugaji wafuge kwa kuzingatia utunzaji na uhifadhi wa mazingira, kwani inawezekana" alisema Gillaa.

Alisema kuwa wafugaji wanaweza kuchafua mazingira kwa kumwaga kinyesi cha Mifugo ovyo pamoja na watu wa machinjio wamkuwa wakitupa ovyo uchafu unatokana na Mifugo iliyochinjwa.

Aidha Gillaa alisema wamekuwa wakitoa ushauri kwa wafugaji wafuge kwa kutima Mifugo chotara kwani ndio Wana himili mabadiliko ya Tabia Nchi yanayotokea.

"Mifugo ya chotara ni mchanganyiko wa mbegu ya kisasa na kienyeji, hivyo mchanganyiko huo unahimili mabadiliko ya Tabia Nchi hali inayopelekea Mifugo kuwa na Afya na kutoa maziwa mengi", alisema Kaimu Mkurugenzi huyo.

Kaimu Mkurugenzi huyo alisema katika kuhakikisha wafugaji wanapata malisho mazuri,Wizara ina mashamba ya kuzalisha mbegu Bora za malisho ambazo wamekuwa wakisambaza katika maeneo mbalimba hapa nchini.

Tanzanite Uk. 2
Tarehe 04/06/2021

Scanned with CamScanner

UHURU UK 3

# Kishimba ashauri benki zikubali ngo'mbe watumike dhamana ya mikopo

Kahama
SALVATORY NTANDU

MBUNGE wa Jimbo la Kahama Mjini (CCM), Jumanne Kishimba ameziomba taasisi za fedha kukubali kupokea mifugo kama dhamana kutoka kwa wafugaji wanaotaka kukopa fedha kwa lengo la kujikwamu kiuchumi.

Akizungumza kwa niaba ya wafugaji wa jimbo hilo wilayani hapa, Kishimba alisema taasisi za kifedha zinapaswa kuweka utaratibu maalumu utakaowawezesha wafugaji wa ng'ombe kupatiwa mikopo kwa kutumia ngo'ombe kama dhamana kuwawezesha kufanya ufugaji wa kisasa.

"Kama mfugaji anatumia ng'ombe kutoa mahari kisha kupewa mwanamke akaoa na kukaa naye maisha yake yote. Kwa nini taasisi hizi zisitoe mikopo kwa wafugaji kuweka dhamana ya mifugo yao ili kujiendeleza kiuchumi," alisema Kishimba.

Alifafanua kuwa sekta mifugo ni sehemu ya uchumi wa taifa, hivyo inapaswa kuandaliwa mazingira mazuri kwa kuwapatia mikopo wafungaji ili wazalishe kufuga mifugo yenye afya nzuri.

Pia, aliziomba taasisi hizo kubuni njia mbadala za kupata faida kupitia sekta ya mifungo na kuacha utaratibu wa zamani wa kuweka dhamana nyumba na mali zingine.

Kwa upande wake, Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Dk. Philimon Sengati, alisema kuwa serikali itaendelea kuondoa vikwazo na kuweka mazingira bora ya biashara kwa wawekezaji hususan wazawa ili kuchangia pato la taifa.

"Shinyanga ina fursa nyingi za kiuchumi, serikali itaendelea kuwasaidia kwa kushirikiana na taasisi zote za umma na binafsi kwa wanaotaka kuwekeza ili mkoa wetu usonge mbele," alieleza.

Mwenyekiti wa Chama Cha Wafugaji Tanzania (CCWT), Jeremia Wambura, alisema hoja ya kuwapa mikopo wafugaji kupitia dhamana ya mifugo ni nzuri na kwamba anaiunga mkono kwa asilimia mia moja.

Alisema mikopo hiyo itawawezesha wafugaji kufuga mifugo yenye tija na kuwekeza katika miundombinu ya umwagiliaji kwenye maeneo yao ya ufugaji.

Scanned with CamScanner

UK 16

# Serikali kuendelea kufanya tafiti za malisho ya mifugo nchini

**Na Omary Mtamike, Tanga**

MKURUGENZI wa Utafiti, Mafunzo na Ugani kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dkt. Angelo Mwilawa amesema kuwa Serikali inakusudia kuendelea kufanya utafiti zaidi wa malisho ya mifugo baada ya kuona matunda ya tafiti ambazo zimeshafanyika.

Dkt.Mwilawa alisema hayo jana jijini Tanga kwenye Mashamba ya Taasisi ya Utafiti wa Mifugo nchini (TALIRI) alipokuwa akiongoza timu ya wafugaji na wazalishaji wa malisho ya mifugo kutoka mikoa ya Njombe, Mbeya, Tanga na Kilimanjaro ambao walifika kwenye mashamba hayo kwa lengo la kujifunza juu ya aina mbalimbali za mbegu za malisho yanayostawi maeneo yenye mvua na yale yanayostahimili ukame.

"Kiu kubwa ya Serikali ni kuhakikisha changamoto ya upatikanaji wa malisho kwa wafugaji wetu inamalizika kabisa na tunapata faraja kubwa pale tunapowaona wafugaji wetu wananufaika na matunda ya tafiti mbalimbali za malisho ambazo tumekuwa tulizifanya kwa kushirikiana na wadau mbalimbali" amesema Dkt. Mwilawa.

Aidha Dkt.Mwilawa alibainisha kuwa ziara hizo za wafugaji zitaisaidia Serikali kupata maoni yao juu ya mambo ambayo wangependa yafanyiwe kazi ili waendelee kuwa na ufugaji na uzalishaji malisho wenye tija na utakaowanufaisha zaidi.

"Napenda niwashukuru wadau wetu ambao wamekuwa nasi katika kufanikisha tafiti mbalimbali zinazolenga kuwasaidia wafugaji wetu likiwepo shirika la "CIAT" na sisi kama Serikali tunawaahidi tutaendeleza yale ambayo wametusaidia hata mara baada ya mradi kuisha" ameongeza Dkt. Mwilawa.

Akizungumza kwa niaba ya wenzake,Suzana Nyagawa ambaye ni mfugaji kutoka mkoa wa Njombe amesema kuwa amefurahishwa na nyingi za malisho ya mifugo alizozikuta shambani hapo ingawa amebainisha kuwa changamoto ya hali ya hewa ya baridi iliyopo kwenye mkoa wake ni moja ya changamoto zinazofanya aina nyingi za malisho zisistawi vizuri.

"Kutokana na changamoto hiyo huwa tunakata malisho tuliyoyapata wakati wa masika kisha tunayakata na kuhifadhi ili yatusaidie wakati wa kiangazi" aliongeza Nyagawa.

Kwa upande wake Gwamaka Mwakiambiki ambaye ni mfugaji kutoka Wilaya ya Rungwe mkoani Mbeya, amesema kuwa jambo alilojifunza mara baada ya kufika shambani hapo ni kuzalisha aina nyingi za malisho ya mifugo badala ya kutegemea aina moja tu ya majani aina ya "brachiaria" ambayo ndio yanayostawi vizuri katika mkoa wake.

"Tunalishukuru sana shirika la CIAT kwa sababu tangu lilipokuja tumejifunza namna ya kupanda malisho bora na yanayoipa mifugo yetu afya bora" alihitimisha Mwakiambiki.

Wizara ya Mifugo na Uvuvi imekuwa ikishirikiana na mashirika mbalimbali ya kimataifa kwenye tafiti za malisho ya mifugo ikiwa ni jitihada za kumaliza changamoto ya malisho ya mifugo nchini.



**Mkurugenzi wa Utafiti, Mafunzo na Ugani kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dkt. Angelo Mwilawa (aliyechuchumaa) akitoa maelezo kuhusu malisho ya nyasi aina ya "buffel au "Cenchrus ciliaris" kama yanavyojulikana kitaalam wakati wa ziara ya wafugaji na wazalishaji wa malisho kutoka Njombe, Mbeya, Tanga na Kilimanjaro iliyofanyika kwenye ofisi za Taasisi ya Utafiti wa mifugo (TALIRI) jijini Tanga jana.** (Na Mpigapicha Wetu)

## Walalamikia uhaba wa magari ya kusafirishia abiria Njombe

**Na Mwandishi Wetu**

WAKAZI wa Kata ya Milo wilayani Ludewa mkoani Njombe wamelalamikia uhaba wa magari ya kusafirishia abiria kutoka Njombe mpaka Milo kutokana na ubovu wa barabara hiyo na kupelekea kutumia gharama kubwa ili kuweza kusafiri na kukwamisha usafirishaji wa mazao.

Wakitoa malalamiko hayo katika mkutano wa hadhara ulioandaliwa na diwani wa kata hiyo Robert Njavike na kuhusisha viongozi wa vijiji na serikali wa kata hiyo uliolenga kusikiliza kero mbalimbali walizonazo wananchi wa kata hiyo.

Jackson Mgimba ni mmoja wa wananchi hao alisema kuwa awali magari yalikuwa mengi na walikuwa wakisafiri kwa gharama ya shilingi elfu tano hadi sita lakini kwa sasa wanasafiri kwa elfu 12 hadi 15 hivyo wanashindwa kusafiri na kusafirisha mazao yao ya biashara.

"Huku magari ni shida sana kutokana na ubovu huu wa barabara ambapo kwa sasa kuna gari moja tu! ambalo halikidhi mahitaji ya wananchi kutokana na wingi wetu, hivyo tunaomba serikali itutengenezee barabara ili tuweze kusafiri kwa gharama nafuu kama wenzetu wa maeneo mengine". Alisema Mgimba.

Naye Edward Mwinuka ambaye

Scanned with CamScanner

Tarehe 04.06.2021

MAZINGIRA

MWANANCH UK 19

# Uharibifu wa mazingira wapunguza samaki Mtera

Lwitiko Mwamakula, Mwananchi

Mpwapwa. Baraza la Madiwani wilayani Mpwapwa limeelezwa uharibifu wa mazingira kwenye Bwawa la Mtera umesababisha upungufu wa samaki na kushuka mapato ya halmashauri.

Hayo yalielezwa na diwani wa Mtera, Robert Maulya kwamba kutokana na uharibifu wa mazingira, samaki wamepungua na hivyo kushusha mapato ya halmashauri yanayotokana na uvuvi wa samaki.

Alisema kutokana na hali hiyo, kuna haja ya kuunganisha nguvu kati ya wanasiasa, jamii na viongozi wa Serikali kupambana na uharibifu wa mazingira ili kunusuru bwawa hilo.

Diwani huyo alisema wanasiasa pia wanatajwa katika uharibifu wa mazingira wa moja kwa moja au wa kuwakingia vifua wale wanaohusika katika uharibifu huo.

Mwenyekiti wa halmashauri hiyo, George Fuime alisema kwa sasa Mpwapwa ni miongoni mwa wilaya ambazo zimeanza kuathirika moja kwa moja na matokeo ya uharibifu wa mazingira, ikiwamo kutanuka kwa korongo la Shaban Robert linalosababisha baadhi ya nyumba za watu kusombwa na miundombinu ya madaraja na barabara kuharibika kwa kiasi kikubwa.

"Kwa hali ilivyo ni lazima jamii na viongozi kuanzia ngazi za chini kupambana na uharibifu wa mazingira."

Mkuu wa Wilaya ya Mpwapwa, Jabir Shekimweri



Hivyo alisema ni lazima kama wilaya kuongeza nguvu katika utunzaji na uhifadhi wa mazingira kwa kushughulikia vyanzo vikuu vya tatizo hilo. Kwa upande wake, Mkuu wa Wilaya ya Mpwapwa, Jabir Shekimweri alisema kwa hali ilipofikia ni lazima jamii na viongozi wote kuzungumza lugha moja katika utunzaji wa mazingira katika wilaya yake.

Alisema historia inaeleza Wilaya ya Mpwapwa ilikuwa inaongoza kwa kuwa na mazingira rafiki na mazuri kutokana na misitu mikubwa, hali ya hewa nzuri ambayo iliwafanya wakoloni kujenga ngome yao humo.

Pia alisema usimamizi mbovu wa sheria unashawishi waharibifu hao kutokuwa na woga wa kutenda makosa, siasa mbovu, rushwa kwa baadhi ya watendaji na kuyafumbia macho matendo hayo.

Alisema mikakati ya wilaya ni kuunda kamati za udhibiti wa uharibifu wa mazingira kuanzia ngazi ya serikali za vijiji na kuanzisha mahakama inayotembea ili kuongeza kasi ya utoaji adhabu kwa wahusika.

Scanned with CamScanner

# Wafugaji watakiwa kufuata Kanuni za ufugaji- Serikali

**NA IMMACULATE RUZIKA-DODOMA**

SERIKALI kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi imewashauri wafugaji wafuge kwa kuzingatia Kanuni za ufugaji ili kukabiliana na mabadiliko ya Tabia Nchi.

Aidha Wizara hiyo imewataka wafugaji kuacha kufuga kiholela kwani Mifugo ikiachwa hovyo usababisha mmomonyoko wa udongo na uchafuzi wa mazingira.

Akizungumza katika maonesho ya Wiki ya mazingira yanayoendelea Jijini hapa Kaimu Mkurugenzi Msaidizi Ugani Mifugo wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi Dkt. Kejeri Gillaa alisema wamekuwa wakitoa Elimu kwa wafugaji yankutunza mazingira.

" Sisi kama Wizara husika,tumekuwa tukitoa elimu kwa wafugaji wafuge kwa kuzingatia utunzaji na uhifadhi wa mazingira, kwani inawezekana" alisema Gillaa.

Alisema kuwa wafugaji wanaweza kuchafua mazingira kwa kumwaga kinyesi cha Mifugo ovyo pamoja na watu wa machinjio wamkuwa wakitupa ovyo uchafu unatokana na Mifugo iliyochinjwa.

Aidha Gillaa alisema wamekuwa wakitoa ushauri kwa wafugaji wafuge kwa kutima Mifugo chotara kwani ndio Wana himili mabadiliko ya Tabia Nchi yanayotokea.

" Mifugo ya chotara ni mchanganyiko wa mbegu ya kisasa na kienyeji, hivyo mchanganyiko huo unahimili mabadiliko ya Tabia Nchi hali inayopelekea Mifugo kuwa na Afya na kutoa maziwa mengi", alisema Kaimu Mkurugenzi huyo.

Kaimu Mkurugenzi huyo alisema katika kuhakikisha wafugaji wanapata malisho mazuri,Wizara ina mashamba ya kuzalisha mbegu Bora za malisho ambazo wamekuwa wakisambaza katika maeneo mbalimba hapa nchini.

Scanned with CamScanner